

# Mwongozo wa ulinzi kwa watu wenye Ualbino

(Mbinu madhubuti za kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino)

Tarehe: July 2017 (nakala rasmi)



## **Kitengo cha Ulinzi na Usalama cha CBM**

**Mwandishi:** Tom van Herwijnen (Meneja wa kitengo cha ulinzi na usalama cha CBM)

**Waandishi wenza:** Steve Ritchie (Mkurugenzi RiskVisibility), Dr Julian Eaton (Mshauri wa masuala ya afya ya kiakili, CBM)

**Tafsiri kwa Kiswahili:** Gamariel Mboya

## Contents

Dibaji .....	4
Utangulizi .....	5
Mwongozo wa Usalama kwa watoto wenye ualbino .....	7
Uchanganuzi wa uchunguzi.....	9
Muongozo wa usalama kwa familia.....	10
Muongozo wa usalama katika mikutano .....	11
Muongozo wa ulinzi kwa wasimamizi.....	12
Uratibu wa matukio ya dharura.....	13
Jedwali: Mpangilio wa kuitikia tahadhari au tukio .....	15
Msaada wa unasihi.....	16
Kutoa taarifa kwa mamlaka husika .....	18
Kufanya kazi na vyombo vya habari.....	18
Kutumia mitandao ya jamii pamoja na teknolojia .....	19
Kujifunza kutoka katika janga. ....	19



UNITED NATIONS  
INDEPENDENT EXPERT  
PERSONS WITH ALBINISM



### **Michango ya mawazo:**

Ikponwosa ERO – Mtaalamu wa Kujitegemea wa Umoja wa Mataifa katika masuala ya Ualbino (UN Independent Expert / Albinism), Dr. Patricia Lund, - Mtafiti wa masuala ya ualbino Chuo kikuu cha Coventry (Albinism Researcher, Coventry University) and Andrew Kain, - Mshauri wa kujitegemea wa masuala ya usalama (Independent Security Consultant), Michael Mwendwa (CBM) and Dr. Manfred Mörchen, - Mtaalamu wa masuala ya macho (CBM Ophthalmologist)

**Onyo:** Baadhi ya vipendele katika mwongozo huu, havifai **kusomwa mbele ya watoto**. Mwongozo huu unaweza kuwa sio sahihi kusomwa kwa mtu ambaye ameathiriwa na vitendo vya ukatili. Hakikisha kuwa makini wakati unatumia mwongozo huu kwa kuzingatia hadhira husika.

Baadhi ya sentensi zimewekewa **maandishi mkolezo** ili kusaidia usomaji kwa watu wenye uoni hafifu.

**Hakimiliki © 2017 CBM** CBM itaruhusu matumizi ya mwongozo huu, kwa sharti la kupata kibali kwa maandishi, kwa kuzingatia kutobadilisha maudhui au kudurufu muongozo huu kwa namna ambayo itapotosha wasomaji. Muongozo huu usitumike kibiashara. Iwapo muongozo huu utachapishwa au kutafsiriwa sentensi ifuatayo inatakiwa kuwekwa “Chapisho la kwanza liliaandaliwa na CBM. CBM ni Taasisi ya kimataifa ya kikristo, ambayo imejikita kuboresha maisha ya watu wenye ulemavu katika jumuiya maskini Ulimwenguni bila ya kujali rangi, jinsia au Imani ya kidini” **[www.cbm.org](http://www.cbm.org)**.

Kwa mawasiliano Zaidi tafadhali wasiliana nasi kwa barua pepe [hssunit@cbm.org](mailto:hssunit@cbm.org)

## **Dibaji**

Nimeshtushwa sana na ripoti za ukatili dhidi ya mamia ya watu wenye ualbino katika mataifa 27 ndani ya miaka 10 iliyopita. Ukatili huu umesababisha mauaji, ukataji wa viungo na athari za kisaikolojia katika maeneo mengi. Halikadhalika hizi ni ripoti za matukio yaliyoripotiwa tu. Inaaminika kuwa matukio mengi yanatokea bila kuripotiwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhusika wa wanafamilia na ukosefu wa mfumo wa ufuatiliaji na utoaji wa taarifa sahihi juu ya matukio ya ukatili. Hali hii inahuzunisha sana. Shukrani kwa juhudi zote zinazofanywa kukomesha ukatili ambazo zimekuwa zikiendelea ikiwemo kuwepo kwa nafasi ya mtaalamu huru katika ofisi ya kamishna wa haki za binadamu Umoja wa Mataifa. Chini ya wadhifa huu, nimeweza kuanza kufanya kazi na wadau mbalimbali katika kutengeneza mikakati madhubuti ikiwemo kujenga miundombinu mahsusi ya kulinda na kuinga vitendo vya kikatili ambazo zitaweza kutumika katika nchi zinazoendelea.

Kwa muktadha huu, napenda kukaribisha Mwongozo huu kwa watu wenye ualbino ulioandaliwa na CBM. Mwongozo huu unatoa njia halisi za kujilinda kwa watu wenye ualbino huku ikitoa mwongozo kwa walimu na walezi. Kwa utaalamu wa CBM katika Nyanja za watu wenye uoni hafifu- hali ambayo watu wenye ualbino huwa nayo- muongozo huu umejikita Zaidi katika hili eneo. Pia umelenga kuiwezesha jamii juu ya mbinu za kuwalinga wana jamii wenzao wenye ualbino. Juhudi hizi zitasaidia kutokomeza hofu ambayo inawakumba watu wenye ualbino katika masuala ya ukatili. Ni Imani yangu kuwa muongozo huu utakuwa sehemu ya uraghibishi baina ya watu wenye ualbino pamoja na kutoaa mafunzo kwa walezi wote wanaohusika na watu wenye ualbino katika mataifa yote yaliyoathirika na ukatili na unyanyapaa. Natarajia kuona mwongozo huu ukisambazwa kwa wingi sana.



## **Ikponwosa Ero**

Mtaalamu huru wa masuala ya Haki na Binadamu kwa watu wenye ualbino

-----

Kwa miaka mingi CBM imekuwa ikisaidia program za watu wenye matatizo ya uoni. Miongoni mwa wateja wetu, tumekutana na watu wenye ualbino; tumesikia hadithi zao, na tumefanya kazi pamoja nao katika kutatua changamoto zao na kutumia fursa za kuleta mabadiliko chanya katika maisha yao na jamii wanazotokea. Tunasikitika sana kuona na kusikia matukio ya kutisha dhidi ya watu wenye ualbino yakiendelea kutokea mpaka leo.



Ni matumaini yetu kwamba mwongozo huu utawawezesha wazazi, shule na jamii katika kulinda watu wenye ualbino ili kula mtu afikie malengo yake kikamilifu.

## **David Bainbridge**

Mkurugenzi wa Kimataifa wa CBM (International Director CBM)

## Utangulizi

Ukatili dhidi ya watu wenye ualbino umekuwa ukitokea kwa miaka nyingi ikiwemo, uonevu, kuita majina mabaya, kutengwa na familia, pamoja na unyanyapaa katika kila ngazi kwenye jamii umekuwa ukiripotiwa. Hivi karibuni kumekuwa na aina ya kipekee ya ukatili. Watu wenye ualbino wamekuwa wakiwindwa na wahalifu kwa misingi ya Imani za kishirikina na Imani potofu kwamba viungo vya watu wenye ualbino vina uwezo wa kimujiza kama zitatumika katika uchawi na madawa ya kienyeji. Kwa bahati mbaya imani hii potofu imeenea sana matika maeneo ya chini ya jangwa la sahara. Pia kumekuwa na Imani hatarishi kwamba vingo vya watoto ndio madhubuti Zaidi katika ushirikina, na kwamba kufanya mapenzi na mwanamke mwenye ualbino kunatibu maambukizi ya virusi kwa mtu aliathirika.

This violence, often leads to traumatizing, maiming and killing of people with albinism. It happens at a local level by perpetrators (sometimes with involvement of a relative). Body parts are reportedly worth high amounts of money on the black market within affected countries. However, some cases indicate cross-border activity which warrants calls for a coherent security strategy both at the grassroots and regionally.

Ukatili hupelekea maumivu ya kihisia, kujeruhiwa na kuuwawa kwa watu wenye ualbino. Hii hutokea katika jamii na wahalifu (nyakati nyingi ndugu wa karibu huhusika) Viungo vya watu wenye ualbino vimeripotiwa kuuzwa kwa thamani kubwa jambo lililoathiri nchi nyingi. Hata hivyo baadhi ya kesi za ukatili zimehusisha uhalifu unaovuka mipaka ya nchi jambo ambalo linatoa wito wa kuwa na mikakati imara ya kiulinzi toka ngazi ya chini mpaka kikanda. Madhumini ya mwongozo wa ulinzi na usalama kwa watu wenye ualbino ni kutoa ushauri madhubuti na halisia kwa watu wenye ualbino pamoja na wale wanaofanya kazi pamoja. Ili kubaki salama katika muktadha wa maeneo wanayoishi. Pia inatoa njia za kitaalamu na hatua rahisi za namna ya kukabilia na matukio na kwa haraka kuratibu rasilimali za kusaidia wahanga wa ukatili kuwa salama.

### Ualbino ni Nini?

Ualbino ni hali adimu, isiyoambukiza, inayorithiwa, hali inayotokea duniani kote bila kujali rangi, kabila au jinsia. Hali hii ni matokea ya ukosefu wa rangi asili katika nywele, ngozi na macho. Baadhi ya athari zitokanazo na ualbino ni hatari ya kuathiriwa na saratani ya ngozi pamoja na uwezekano mkubwa wa kuwa na uoni hafifu. Mara kwa mara hukabilia na maneno machafu na hivi karibuni ukatili katika miili yao. Ili mtoto azaliwe na ualbino, ni lazima wazazi wote wawe wamebeba vinasaba vinavyosababisha ualbino hata kama wao hawana ualbino unaoonekana kwa nje. Uwepo wa ualbino unatofautiana maeneo mbalimbali ulimwenguni. Kwa mujibu wa shirika la afya duniani, makadirio ya uwiano yanatofautiana kutoka mtu 1 kati ya watu 5,000 hadi mtu 1 kati ya watu 15,000 chini ya jangwa la sahara. Huku baadhi ya makundi yakiwa na uwiano mkubwa wa mtu 1 kati ya watu 1,500. Ulaya na Amerika ya kaskazini, inakadiriwa mtu 1 kati ya watu 17,000 mpaka 20,000 ana ualbino.



### Ukweli mchungu

Mnamo tarehe 4 Mei 2013, wataalamu mbalimbali wa umoja wa mataifa walisisitiza kuwa katika baadhi ya maeneo ya nchi za Africa, zinaamini kuwa viungo vya watu wenye ualbino vina nguvu za kimiujiza ambayo huweza kuleta utajiri. Kama vikitumika katika madawa ya kienyeji yanayotengenezwa na waganga wa kienyeji. Wengine wanaamini kuwa uchawi una nguvu Zaidi ikiwa mhanga atapiga kelele wakati akiwa anakatwa kiungo chake. Kwahiyo viungo hukatwa wakati mhanga yupo hai.

Tangu mwaka 2000, asasi za kijamii zimeripoti matukio ya ukatili 450 ya watu wenye ualbino katika nchi 25 barani Africa. Zaidi ya watu 170 wenye ualbino wamepoteza maisha kutokana na ukatili na wengine wengi wamekatwa viungo vyao au kubakwa.

wa matukio ya kikatili.

Barani Africa watu wenye ualbino hutambulika kirahisi kutokana na mwonekano wao, hasa wangi ya ngozi hivyo kuweza kuonekana kirahisi. Wengi wao hupata shida ya uoni hafifu hali ambayo inaongeza athari kwao. Uoni wao hafifu hupelekea watoto wenye ualbino kupelekwa shule maalum za wasioona jambo ambalo linapelekea kuweza kuwindwa kirahisi.

Katika utendaji wake, CBM imefanya kazi kwa miaka mingi katika usimamizi wa Ulinzi jumuishi katika masuala ya ulemavu pamoja na mafunzo ya ulinzi. Kutokana na ujuzi huu pamoja na mchango wa watu mbalimbali wenye ulemavu, mbinu mbalimbali nan a utalamu umeandaliwa. Hii inahusisha kuzuia matukio na kukinga matukio ya kikatili pamoja na kuratibu kwa haraka mfumo wa kusaidia wahanga

Tunaamini kwa dhati kuwa maamuzi jumuishi katika kutatua tatizo tunalolikabili, itapelekea kuwa na uelewa mpana, matukio machache na mfumo thabiti wa usimamizi. Ingawa kumekuwa na kupungua kwa ukatili katika maeneo ambayo matukio haya yalitokea kwa wingi hado hatuwezi kujiridhisha na kukaa kimya kwakuwa bado juhudi za kuchimbua kiini cha sababu za ukatili na Imani potofu dhidi ya watu wenye ualbino hazijakidhi mahitaji. Uhalifu huu unaweza kuvuka mipaka na kutekelezwa katika nchi zingine.

Kutokana na **kuongezeka kwa uelewa, mafunzo na jitihada**, itawezesha:

- **watu binafsi, wazazi, waalimu pamoja na walezi** watawezesha kutambua changamoto na kutoa mwitikio sahihi.
- **Watoto wenye ualbino** watatambua hali za hatari mapema na kuchukua hatua za haraka.
- **Makundi rika** yatachukua wajibu kwa kila mmoja na kupata uhifadhisalama baina yao katika kundi.

### Kutambua Hatari.

Jifunze kutambua mazingira yanayokuzunguka. Chunguza kutambua vitu na matukio ambayo sio ya kawaida mfano:

Kuna mtu nimemuona mara kadhaa kabla, kwanini mtu huyu/gari linafuatilia? kwanini watu hawa watatu wanakaa ndani ya gari kwa muda mrefu karibu na nyumbani ninapotoka kwenye basi la shule?

Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kwa watu wenye ualbino

- **Wanafamilia na jamaa** watachukua wajibu wa kuhakikisha wanafika salama katika maeneo ya shule na kazi.
- **Walinzi mashuleni** na kwenye taasisi wataweza kutambua watu Watawala watachukua hatua kwa haraka pale matukio yanapotokea.
- **Jamii** itaunganisha nguvu kushughulikia tatizo linapotokea.
- **Jamii** pamoja na **viongozi wa dini** watakemea vikali matukio ya ukatili pamoja na kukusanya rasilimali kuwezesha kutatua changamoto.

Nakualika kusoma mwongozo huu na kufanya maamuzi ya makusudi ya kutekeleza hatua rahisi na zisizo gharimu za kusaidia kulinda watoto na watu wenye ualbino. Katika kufanya hivi, utakuwa umechangia katika kulinda maisha ya thamani na kuleta tofauti katika maisha ya watu wenye ualbino Tafadhali sambaza chapisho hili katika UN, AZAKI na watu wenye ualbino pamoja na mtandao wa mashirika ya watu wenye ulemavu pamoja na taasisi za haki za binadamu.

Iwapo una maswali Zaidi kuhusiana na ulinzi wa watu wenye ualbino, Ulinzi na usalama shirikishi na mafunzo, mafunzo kwa AZAKI juu ya mifunzo ya ulinzi tafadhali wasiliana na [hssunit@cbm.org](mailto:hssunit@cbm.org)

## Mwongozo wa Usalama kwa watoto wenye ualbino

Watoto wenye ualbino hudhaniwa kuwa katika hatari kubwa. Watoto ni wadogo na hawana nguvu ta kujilinda pamoja na kuwa na uoni hafifu, wanaweza wasitambue kama kuna watu wanawaangalia au kuwafuata. Watoto wengi huenda shule kwa kufuata ratiba za kawaida kama wengine. (muda, sare za shule na njia za kupita) ni rahisi kuwindwa, kufuatiliwa na kulengwa hasa katika maeneo yaliyojitenga. Baadhi ya wazazi wameamua hata kuwatoa watoto wao wenye ualbino mashuleni kwa kuhofia usalama wao wanapokuwa wanaenda shuleni.

### Msimu wa Mvua

Familia moja huko Malawi karibu na ziwa ilisema kunakuwa na hatari Zaidi nyakati za mvua wakati watoto wanaporejea kutoka shule pale wanapoomba hifadhi wanapojikinga na mvua.



Zifuatazo ni hatua muhimu za kufuata na kujadiliwa kwa watoto wenye ualbino, familia zao, walezi na wale ambao wapo masomoni.

- **Epuka kutembea peke yako** uendapo shule: Hakikisha kuwa unapokwenda shule au kurudi nyumbani, unatembea na marafiki unaowaamini ambao kazi yao ni kuhakikisha unafika nyumbani salama.
- **Kutengeneza mfumo wa makundi rika shuleni:** inapowezekana, baadhi ya vijana walioaminiwa wanaweza kuungana na watoto wenye ualbino kusaidiana, kuhakikisha wapo salama na kuweza kuwa makini katika kuhakikisha usalama.
- Inapowezekana **badilisha mida ya kwenda shule na kurudi nyumbani**, epuka kutumia njia moja au ratiba ambazo wahalifu wanaweza kukisia.
- **Epuka kutembea njia ambazo zimejitenga.** Tembea nyakati za mchana
- Jifunze kutathmini uhalisia wa mazingira na kutambua hatari.
- **Tembea na filimbi yenye Kamba kuzunguka shingo:** Ipulize kwa nguvu pale unapohisi hatari.
- **Jifunze kuamini hisia zako-** Unapohisi hujisikii vizuri lazima kuna sababu zake. Fanya maamuzi haraka bila kusita.
- **Usikubali kupanda gari kusaidiwa kufika mahali:** hii ni hata kwa mtu unayemfahamu, tumia hisia zako kikamilifu, Usiamini mtu kirahisi hata akikuambia mfano” mama yako amenituma nikuchukue”
- **kuwa makini na wageni** au watu ambao wanakufuatilia, epuka kuwa karibu nao
- Jizoeshe kutoa taarife unaposafiri: **mwambie rafiki unaemwamini maeneo unayoenda.** Elezea namna utakavyoenda na wakati unaotegemea kufika. Kama una simu tuma ujumbe mfupi wa maneno muda unapoondoka/kufika (m.f WhatsApp) muombe rafiki yako kufuatilia mwenendo wako na ambapo utahitaji kutoa taarifa endapo hujafika kwa wakati au kwa muda uliotarajiwa na mahali husika

### **Kukabiliana na Utafwaji**

.mara kwa mara wataalamu wa usalama hushauri wahanga wa utefwaji wasioneshe pingamizi wakati wanapotekwa ili kuongeza fursa ya kuwa hai. Hata hivyo, dhamira za watekaji wa watu wenye ualbino inachagizwa na thamani viungo vya watu wenye ualbino ambavyo hupelekea vifo. Kwa muktadha huu inashauriwa kwamba wakati inapotokea jaribia la kutekwa, jikinge na kupiga kelele za kuomba msaada kwa matumaini kuwa kelele hizo na kujikinga kutasaidia kupata msaada wa haraka. Kujikinga kwa mhanga kutamlazimisha mtekwaji kumuachilia mhanga. Unaweza ukaumizwa lakini ukaongeza uwezekano wa kuwa hai.

### **Julai 2016, Tanzania**

Shule moja jumuishi ya sekondari ina watoto 15 wenye ualbino wanaoishi katika bweni. Mkuu wa shule anaeleza kuwa shule ni kubwa (Walimu 70 na wanafunzi 1400) na wote wamefundishwa juu ya hitaji ya kuwalinda wenzao wenye ualbino. Wao ni “macho yao”.



- Katika zile njia unazopita mara kwa mara **hakikisha kuwa unajua maeneo salama ya kukimbilia** iwapo utahitaji kujihifadhi kama kuna mazingira hatarishi.

#### **Muhimu kwa wasimamizi mashuleni**

- **Hakikisha madereva wa mabasi ya shule na walinzi wamefundishwa** na kupewa jukumu la kulinda na kuwatetea watoto wenye ualbino.
- Hakikisha watoto wote wameelekezwa **mbinu za kutoa taarifa** na nani wa kumppa taarifa endapo tukio litatokea.
- Zingatia kuwafundisha watoto wote **masomo ya ukakamavu** ambapo wanajifunza kuwa imara, kutambua mipaka na alama za hatari na kuwawezesha kutoa taarifa. Hii inaweza kuhusisha mbinu muhimu za kujikinga endapo watavamiwa.

#### **Ualbino na Uziwi Tanzania**

Imebainika kuwa idadi kubwa ya wanafunzi wenye ualbino, wanakabiliwa na tatizo la masikio. Ili kuwezesha uwezo wao wa kubaini hatari katika mazingira, ni muhimu kufanya vipimo vya uziwi na kutoa vitendea kazi husika.



Malelezo ya hapo juu, yamewalenga watoto. Ingawa ushauri uliotolewa unafaa pia hata kwa wanawake au watu ambao wameathirika na ulemavu.

#### **Uchanganuzi wa uchunguzi**

Katika maelezo hapo juu, baadhi ya misingi imeainishwa ili kumsaidia mtoto kutambua mambo ambayo yanatokea isivyo kawaida. **Imethibitishwa kuwa wahalifu wengi hufanya uhalifu baada ya kutumia muda mwingi katika uchunguzi.** Wahalifu hawafanyi uhalifu wao kwa kubahatisha. Huhakikisha **wanapunguza uwezekano wa kutambuliwa na kukamatwa kwa kutafuta njia rahisi ya kuwafikia wahanga.** Wahalifu hutafuta mbinu za kungeza nafasi za kufanikishauhalifu wao kwa kujua eneo, kutafuta urahisi wa kufanya

uhalifu, kwa kujua ratiba za mhangana na kuvamia wakati ambao mhangana atapatikana kirahisi, akiwa hana habari na asipokuwa na kinga.

Makundi ya wahalifu wanaweza kutembelea maeneo ambayo wanalenga kuwapata wahanga, maeneo haya ni kama shuleni ambapo watoto wenye ualbino wanasoma au maofisini ambapo wanawake na wanaume wenye ualbino wameajiriwa au hupatikana mara kwa mara. Wanaweza kukaaa ndani ya gari karibu na geti la shule ili kuona ni nani anayetoka na anatoka muda gani. Wanaweza kumfuatilia mtu kwa mbali ili kujua njia anazopitia.

**Kwa kutumia mafunzo ya usalama, (shuleni), walinzi, madereva na watu wengine walioaminiwa, wanaweza kufundishwa kutambua**

**hatari.** Walinzi wanatakiwa kuwa makini kila wakati, wakishika doria katika maeneo yao na kufanya maamuzi ya haraka pale wanapotambua kuna uwezekano wa hatari kutokea. Wanapaswa kutambua ya kuwa muda wote ni kwa nani na namna gani wanaweza kutoa taarifa, wanatakiwa kushirikisha utoaji wa taarifa kwa jambo lolote ambalo wana wasiwasi nalo na kutoa hatua madhubuti za kuwalinda watoto ambao wapo chini ya hifadhi zao.

### **Muongozo wa usalama kwa familia**

Unapokuwa na mwanafamilia mwenye ualbino, ni muhimu kuhakikisha kuwa makini na uhalisia wa mazingira pamoja na kutambua mazingira hatari. Usifikirie kuwa hatari na huzuni haziwezi kuifikia familia.

Kwa bahati mbaya, baadhi ya watu wanaosukumwa na fikwa na kupata pesa au Imani za kishirikina, wanakosa weledi wa dhamira na kufikiria kuwa mwanafamilia anaweza kuwa chanzo cha utajiri wa haraka au kuleta bahati. Kutaokana na uchambuzi wa matukio ya ukatili, inaaminika kuwa upotevu wa watu wenye ualbino unakuwa umepangwa na, au kuwepo kwa uhusika wa mwanafamilia au jirani ambaye anajua ratiba za familia na maeneo ambayo wanaweza kupatikana kirahisi.

Tunawaasa wazazi **kuwa tayari kuzungumzia masuala yahasuyo ualbino.**

- Watunze watoto wako wenye ualbino vizuri. Jifunze juu ya mahitaji yao na tambua namna ya kuelezea namna ambavyo ualbino ni hali ya kurithi pamoja na hao wanaowazunguka.

#### **Makazi salama**

Kumekuwa na matumio ya makundi ya wahalifu wakiwa na mapanga ambao wanatokea nyakati za usiku wakitaifuta kuwateka watoto wenye ualbino. Malengo yao ni kuangalia njia nyepesi na haraka ya kuteka. Zingatia kuweka vingingiti ambavyo vitaondoa urahisi wa kuvamiwa. Tafuta namna ya kuwazuia wahalifu (mfano makufuli mazuri, kuweka mbwa, milango imara au chumba salama) weka mfumo wa king'ora. Kubaliana na majirani kuwa mtakuwa mkiangalia usalama wa kila mmoja wenu.

Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kwa watu wenye ualbino

- Jadili kwa uwazi mahali ambapo unahisi hatari ipo na chukua maamuzi ya haraka.
- Kuunganisha jumuiya za kidini pamoja na ndugu na jamaa wa karibu na kwa pamoja kuhakikisha kuwa wanafamilia wenye ualbino wanalindwa huku wakishiriki kikamilifu katika masuala ya jamii.

Watoto wako wenye ualbino **ni wa thamani na wanaweza kuwa na mchango mkubwa katika jamii**. Kwa hiyo hakikisha unawalinda ili waweze kufikia ndoto zao.

### **Kutambua nyakati**

Unaweza kuwa mualizi kwa watu wenye ualbino kwa kuweza kutambua nyakati ambazo wahalifu wanatega mitego ya kuwaketa watu wenye ualbino. Chunguza nyakati salam na nyakati hatarishi.

Tafadhali zingatia mapendekezo yaliyotolewa katika sura iliyoitangulia.

- **Zingatia kufanya tathmini mapema juu ya namna familia yako inaenenda katika ratiba za kila siku, mizunguko na safari.**
- Hakikisha kuwa usafiri salama upo au watu wa kusindikiza mfano wakati wa kwenda shule na wakati wa kurudi shule.
- Zingatia kuweka ulinzi Zaidi nyakati za sikukuu, sherehe au matukio ambayo watu wengi wanakushanyika au wanaoingia na kutoka katika eneo Fulani
- Epuka kuwaacha watoto wenye ualbino chini ya uangalizi wa mtu ambaye humuamini hata kidogo. Umuamini mtu ambaye ana historia za kiuhalifu au mwenye mawasiliano na wahalifu.

Inapobidi, **unganisha msaada toka kwa jamii** na marafiki na wasiliana na mamlaka za shule kutaka mikakati madhubuti ya ulinzi. Kuwa na watu wengi wanaolelewa, wanaoshiriki na kuwa tayari kulinda watu wenye ualbino, itasaidia kufanya familia kuwa salama.

### **Muongozo wa usalama katika mikutano**

Unapoandaa mkutano ambao watu wenye ualbino watahudhuria, kuwa makini juu ya hatari zinazoweza kutokea kwa ajili yao wanapokuja na kurudi kwenye mkutano.

- **Fanya utafiti kama katika eneo hilo kumewahi kutokea ukatili** (dhidi ya watu wenye ualbino) au kama kuna magenge ya wahalifu katika eneo hilo.
- Tafuta usafiri salama.
- Weka mfumo wa kupata marafiki. Kumbuka kuwa hata wakiwa wawili au zaidi wanaweza wasijikinge dhidi ya wahalifu wenye silaha.
- **Chagua na kukagua mahali salama pa malazi**, ambapo watu watakutana, watakula na kulala bila kuwindwa.
- Zingatia kuandaa usafiri, mfano usafiri kati ya sehemu hoteli na eneo la kukutania.
- **Kila mara chunguza maeneo ambayo wahalifu wanaweza kuvamia na imarisha ulinzi wa kutosha.**

- Zingatia muda wa kuanza na kumaliza kikao ili watu waweze kufika katika maeneo wanayoishi salama kabla giza halijaingia.

**Kwa kila mkutano mkubwa** (mfano, kongamano au warsha) **chagua mtu ambaye atashika dhamana ya ulinzi na mpatie jukumu la kulinda washiriki na kuwa salama.** Hakikisha mtu huyo amewezeshwa (kuwa na simu yengye chaji ya kutosha na muda wa maongezi) na mtandao ambao unapatikana kwa urahisi katika eneo hilo, ili aweze kutoa taarifa na kuratibu kama kuna tukio. Toa jina na namba ya simu ya mhusika wa ulinzi kwa washiriki wote na zingatia kutoa muhtasari wa usalama kuhusu eneo husika na tukio.

### **Muongozo wa ulinzi kwa wasimamizi**

Iwapo wewe ni kiongozi au msimamizi wa mradi, kiongozi wa shule au taasisi ambapo watu wenye ualbino wanafanya kazi, kusoma au kukutana, unapaswa kubeba majukumu ya ziada ili kuhakikisha usalama wa watu waliopo chini yako. Zifuatazo ni njia rahisi zinazoshauriwa na zisizogharimu katika kutekeleza.

- **Teua mtu katika timu yako ambaye atahusika na masuala ya usalama.** Mtu huyo atafanya tathmini ya hatari za usalama kwa watu wenye ualbino.
- **Suala la ulinzi na usalama linatakiwa liwe ajenda ya mara kwa mara** katika mikutano ya menejimenti ambapo mtajadili mwenendo wa matukio na namna yanavyotokea.
- Fanyia kazi haraka iwezekanavyo kuhusu ushauri na mapendekezo
- Andaa mafunzo kwa wanafunzi, wafanyakazi, walinzi na madereva kwa mujibu wa muongozo huu.
- **Wawezeshe watoto walio katika hatari kwa kuwapa filimbi** wavae shingoni
- Andaa **vifaa visaidizi** kama vile miwani ya macho kwa watoto wenye ualbino ili kuimarisha uoni wao hasa katika kuchunguza mazingira yanayowazunguka. Kama vifaa hivi havipo au ni bei sana, miwani ya jua inaweza ikawasaidia.
- **Wajibisha walinzi na madereva, kufanya kazi zao kwa umakini mkubwa** na kufanya doria na kuchunguza mitaa, mageti na uzuio.
- **Weka mfumo wa kutoa taarifa juu ya hatari**, mfumo ambao utapeleka taarifa kuhusu hatari. Watahadharishe watu kutoa ripoti juu ya matukio, hatari ambayo ingetokea na hisia zozote za matukio.
- Weka mfumo na **wasilisha mtandao wa kuripoti** taarifa.
- Angalia kama kuna hatari katika mfumo wa usafiri, angalia njia salama na ratiba za wanafunzi au wafanyakazi.
- **Weka mfumo wa marafiki** na inapobidi andaa mfumo rasmi na usafiri salama.
- **Weka mfumo thabiti wa mahudhurio** ili uweze kujua kila wakati ni nani amefika na ambaye hajafika. Chukua hatua za haraka unapojua kuwa kuna mtu amechelewa kufika au hajulikani aliko.

- **Unapokuwa na Mabweni shuleni:** Mahali ambapo wanafunzi na wafanyakazi wanalala usiku, kwa umakini chunguza hatari zinazoweza kutokea kwa watu wenye ualbino na chukua hatua kulingana na muongozo huu. Zingatia kuangalia uzio wa mabweni na hakikisha kuna makomeo imara katika kila eneo la kuingilia.
- **Andaa mpango wa dharura** iwapo janga litatokea, kwa kuwa na majina, picha za mrithi pamoja na anuani za wanafunzi wote na wafanyakazi. Tunza kumbukumbu hizo mahali salama ili zisitumiwe vibaya.
- **Zingatia kufanya mazoezi ya utayari wakati wa dharura** pamoja na timu yako au tafuta msaada wa kufanya mafunzo ya usalama.
- **Hakikisha kuwa unaboresha daftari lenye mawasiliano** ili kwa haraka uweze kuwafikia polisi, mamlaka katika jamii, viongozi wa dini pamoja na vyombo vya habari

#### Agosti 2016, Malawi

Katika mazingira ya nje huko Blantyre, Majaribio matatu ya kumteka mtoto mwenye ualbino mwenye umri wa miaka 6 yalifanyika ambapo wahalifu walijaribu kumrubuni mtoto huyo kuingia ndania ya gari lao. Mwitikio wa haraka kwa wanajamii waliomzunguka mtoto huyo ulipelekea ukombozi wake.

### Uratibu wa matukio ya dharura

Kwa kawaida, ni vizuri kuwekeza muda wote, nguvu na rasilimali katika mafunzo na kuzuia matukio yasitokee. **Mengi yanaweza kufanyika ili kuzuia matukio ya ukatili.** Hata hivyo matukio ya ukatili yanaweza kutokea, lakini kama kuna utayari wa kutosha na hatua za haraka zikachukuliwa, inaweza kuokoa maisha. Kutokana na uzoefu, tumejifunza kwamba kufanya mazoezi ya utayari huongeza uwezekano wa wahanga wa ukatili kuokolewa bila ya kudhuriwa.

#### **Katika uthibiti wa matukui, hatua za awali ni za muhimu sana.**

Tunaangalia mienendo ambayo imezoeleka zaidi- utekwaji wa watoto wenye ualbino- tunapaswa kukabiliana na uhalisia bila kujali ugumu wa hali

Wahalifu ambao huteka watu wenye ualbino kimsingi huwa na malengo mawili, ukatili wa kijinsia au uhitaji wa fedha. Binti au mwanamke aliyetekwa (nyakati zingine wavulana na wanaume) wanaweza kuwalazimisha kuwabaka na kuwaambukiza ukimwi au kupata uja uzito

Mtu aliyetekwa anaweza kupelekwa katika eneo tulivu punde tu baada ya kutekwa, mahali ambapo anaweza kuuwawa au kukatwa viungo kwa dhumuni la kuviuza. Kwa kadiri wahalifu wanavyosubiri, ndio

#### Malawi, 2013

Katika kijiji kimoja (baba wa kambo alihusika kumteka mtoto wa kike mwenye ualbino) jamii ilihusika kumtafuta mtoto huyo kwa saa sita na kumkuta akiwa amefichwa kwenye shimo baada ya mtekaji kutoroka. Huu ni mfano mzuri wa ujasiri wa mtoto pamoja na jamii katika kuitikia tukio la dharura.



Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kwa watu wenye ualbino

kiwango cha uwezekano wa kugundulika huongezeka. **Kwa sababu malengo ya kuwateka watu wenye ualbino hutofautiana, hivyo hawana muda wa kupoteza.** Hakuna muwa wa majaribio au majadiliano wakati wanafanya uhalifu huo.

Mara chache miongoni mwa wahalifu (au kama mmojawapo ana madeni) anaweza akamteka mtu kwa lengo la kumuiza kwenye magenge ya wahalifu ili apate fedha.

Matukio machache sana ambapo waliotekwa walikutwa wakiwa hai na kutoroka, kwa ujumla jambo moja lilikuwa limefanyika; jamii nzima ilifahamu juu ya tukio na kuandamana kuanza kumtafuta mhanga. Mamia ya watu wakihusika katika kumsaka mhanga, viongozi wa kijamii wakikemea matukio na viongozi wa dini wakiwahimiza waumini wao kusaidia, eneo kubwa hufikiwa na hatimaye mhanga kupatikana na wahalifu kutiwa nguvuni.

Kwa bahati mbaya, ukiachana na mbinu thabiti za kuzuia, kuna njia mbadala za kusitisha majanga.

### **Toa ushirikiano wa haraka kuamsha ushiriki wa jamii.**

1. Tunahitaji viongozi wa kijamii (wabunge, machifu) kukemea vikali).
2. Kuwahimiza ili waikusanye jamii kusaidia kuwatafuta wahanga katika eneo husika.

Jedwali hapo chini litakusaidia kutathmini hali halisi na kuchukua uamuzi wa kukusanya rasilimali za kumsaka mtu aliyepotea

Kupata mtazamo chanya wa jamii ni muhimu sana. Hii itawezekana pale ambapo kuna mifumo madhubuti na maandalizi ya kukabiliana na dharura. Muda unaweza kupotea sana kama wasimamizi watakuwa wanahangaika kutafuta rekodi za mawasiliano. Mwitikio utakuwa wa polepole iwapo watu hawatajikusisha kuwa na mawasiliano mazuri kwenye jamii, na wasipojua yupi katika mamlaka atafaa kufuatwa.

Uongozi unapaswa kuwekeza katika ushirikiano mzuri katika jamii, machifu na viongozi wa kidini na kuboresha mahusiano na mawasiliano nyakati za dharura. Kwa kadiri **unavyokubalika** ndivyo utakavyofanikiwa kuwaunganisha wadau katika kupata msaada wakati wa majanga.



## Jedwali: Mpangilio wa kuitikia tahadhari au tukio

Tahadhari inapotokea ( katika mfumo wowote) juu ya tukio ( mfano; kupotea, kutekwa, mashambulizi) yanayohusisha mtu mwenye ualbino

### aina ya tukio ( la hatari sana )

Hatua za kufanya

- 1 Ainisha taarifa; nani, wapi, nini, lini?
- 2 Thibitisha taarifa kutoka katika chanzo ambazo taarifa zimetokea.
- 3 Tathmini tukio kama ni la kweli au ni tishio.
- 4 tathmini tukio: kama ni la kweli na watu wapo kwenye hatari kwa haraka fanya yafuatayo

### aina ya tukio ( sio hatari sana )

Hatua za kufanya

- 1 Hakikisha usalama wa mtu aliyehusika
- 2 Tambua mafunzo muhimu ( nini ambacho kinaweza kufanywa kwa ubora Zaidi, je kuna muendelezo au kujirudia rudia? )
- 3 Shirikisha masomo hayo kwa wadau na weka mpango wa kuyatekeleza bila kuchelewa

### Kuratibu tukio

hatua za kufanya

- 1 Tuma timu ya watu katika eneo la tukio ili kutathmini sababu na kutambua namna ya kuwasaidia wahanga
- 2 Tengeneza timu ya Majanga ili kuratibu hatua za kufuata wakati wa dharura

### hali za matokeo mazuri




hatua za kufanya

- 1 Iwapo mtu aliyepotea /kutekwa kapatikana, toa huduma za unasihi kwa mhanga (angalia hapo chini).
- 2 Andaa usaidizi wa unasihi kwa familia/ au kundi rika kwa wahanga ( angalia hapo chini)

3	Toa tahadhari na kuwezesha hatua za kiusalama katika jengo na wakati wa usafiri.	3	Tathmini tukio, jifunze namna lilivyodhibitiwa na chunguza athari na mwenendo wake
5	Hakiki usalama wa watu wengine walio katika hatari.	4	Weka katika vitendo mapendekezo bila kusita.
5	Wasiliana na ngazi husika za uongozi kuomba msaada wa haraka.	5	Washukuru wale wote waliosaidia na kuomba ushirikiano Zaidi.
6	wasiliana na viongozi katika jamii husika na kuomba msaada wa <b>MUIMU NA HARAKA.</b>	6	Imarisha mitandao ya kutoa tahadhari na kukuza uelewa wa watu katika kuzuia matukio
7	wasiliana na viongozi wa kidini kuomba msaada wa <b>MUHIMU NA HARAKA.</b>		
8	Wasiliana na familia au mrithi kupata ukweli wa mambo na kuratibu rasilimali		
9	Tumia mitandao ya kijamii kutoa tahadhari na kuomba msaada.		
10	Tathmini tukio kisha jifunze namna lilivyodhibitiwa, angalia athari na mwenendo kisha wekea utekelezaji mapendekezo.		

### **Msaada wa unasihi**

Ni muhimu kwa mtu ambaye amepatwa na athari za kuumiza moyo kupata msaada sahihi kutoka katika familia na jamii inayomzunguka, na ikiwa kuna ulazima, kutoka kwa mtaalamu wa afya ya akili. Baadhi ya kanuni rahisi zinaweza kusaidia kuhakikisha watu wanafaidi kutoka katika mifumo ya usaidizi na kuepuka kupatwa na athari kubwa zitokanazo na majaribio ya kuwasaidia wahanga.

<b>ANGALIA</b>	<ul style="list-style-type: none"><li>• Angalia usalama.</li><li>• Angalia watu wenye mahitaji ya msingi.</li><li>• Angalia watu walio na athari dhahiri za dhiki.</li></ul>	
<b>SIKILIZA</b>	<ul style="list-style-type: none"><li>• Washughulikie watu wanaohitaji msaada.</li><li>• Waulize watu mahitaji yao.</li><li>• Wasikilize watu, na uwasaidie kutulia.</li></ul>	
<b>HUSIANISHA</b>	<ul style="list-style-type: none"><li>• Saidia watu kushughulikia mahitaji ya kimsingi na huduma za ufikikaji.</li><li>• Saidia watu kukabiliana na shida.</li><li>• Toa habari.</li><li>• Unganisha watu na wapendwa wao pamoja na msaada wa kijamii.</li></ul>	

### **Kanuni za kutoa usaidizi wa awazi wa unasihi**

**Angalia:** hakikisha kuwa mhanga yupo mbali na hatari na mahitaji muhimu yamefahamika. Je wapo salama? Je wanahitaji chakula au nguo? Je wapo katika mazingira ambayo wanahisi wapo salama?

Watu ambao wana msongo au matatizo ya kihisia au kushindwa kuwasiliana baada ya tukio kutokea, wanahitaji kupewa muda wa kurudi katika ukawaida. Iwapo wamepata athari kubwa kisaikolojia baada ya muda mrefu, italazimu kupelekwa kwa wataalamu. Hairuhusiwi kulazimisha wazungumzie historia zao iwapo hawataki kufanya hivyo. Jambo hili huthoofidha sana na sio tiba labda mhusika aamue kufanya hivyo.

**Sikiliza:** jambo la muhimu zaidi ambalo linaweza kufanyika kusaidia mhanga alieyathiriwa kisaikolojia ni kuonyesha kuwa upo kwa ajili yao, na kwamba unahusika katika maslahi yao. Onyesha msaada na utayari wa kuwapa muda wa kuwasikiliza, kimsingi marafiki na familia wanaweza kutoa msaada. Kama hujulikani kwa mhanga, jitambulisha na kuwajula hali, kisha waulize kama wapo huru kuongea na wewe ( ikiwezekana katika eneo lenye faragha). Uliza kama wana mahitaji yoyote au dukuduku. Usilazimishe kwa lazima waongee, au kuuliza swali na mkato. Kama wana msongo, watulize na kuwahakikishia kuwa wapo salama. (iwapo kama hilo ni sahihi). Ongea kwa sauti ya chini na kwa utulivu. Hakikisha unamuangalia usoni.

**Husianisha:** wasaidie kutoa madukududku yao na kutathmini mahitaji ya muhimu ambayo wanahitaji. Wahusianishe na familia na marafiki ambao wanaweza kusaidia, waunganishe katika huduma ambazo wanaweza kusaidia kwa muda mrefu eitha kwa vitendo au kwa msaada wa kiafya.

Kwa ujumla ni muhimu unapofuata mapendekezo ya kiusalama, watu wenye ualbino wanaweza kuhusihswa katika majukumu ya kawaida katika jamii. Mapendekezo haya yanapaswa kusaidia watu kuwa salama kuliko kuishi katika hofu. Haipaswi kulaumiwa kutokana na hali na mkazo uwekwe katika kubadili tabia za watu wengine katika jamii.

Unapotoa taarifa ya tahadhari kwa mtoto itasaidia kufanya yafuatayo;

- Wape muda wa kutosha kupokea taarifa.
- Washirikishe taarifa muhimu katika mfumo ambao wanaelewa na wape muda wa kuuliza maswali. Hii ihusishe majadiliano kuhusu lini tukio limetokea au kama kuna tetesi katika jamii au shuleni.
- Hakikisha wasitoe lawama kutokana na hali halisi.
- Kuwa mvumilivu iwapo wataonyesha tabia kama vile kukojoa kitandani, kutokana na hofu ya tukio.
- Usiwatenganishe kutoka kwa wapendwa wao, na wasaidie kuendelea na ratiba zao katika mazingira ambayo wanayafahamu vizuri.

## **Kutoa taarifa kwa mamlaka husika**

Kunaweza kuwa na masiliano katika ngazi ya kitaifa au katika asasi za kijamii ambazo zinaweza kupokea taarifa ili kufuatilia matukio. Kwa kadiri matukio yatakavyoripotiwa katika ngazi za juu, ndivyo itakuwa rahisi kufuatilia kwa karibu mwenendo wa matukio na kufanya tathmini, mamlaka kutaarifiwa, kuchukua hatua na haki kutendeka.

Kwa nyongeza mbali na hatua hapo juu, unapohisi tukio linalohusisha mtu mwenye ualbino, tunashauri **kutuma taarifa** kwa **mtaalamu huru wa umoja wa mataifa anayehusika na haki za binadamu kwa watu wenye ualbino**.

Kupitia [albinism@ohchr.org](mailto:albinism@ohchr.org) au mitandao ya kijamii ya

facebook/Twitter/Instagram: @unalbinism or use Facebook: "UN Albinism".

## **Kufanya kazi na vyombo vya habari**

Wakati janga linapotokea, vyombo vya habari vina mchango mkubwa.

Ushirikishwaji wa vyombo vya habari utasaidia kuleta matokeo chanya.

Ushirikishwaji usio makini kwa vyombo vya habari utapelekea kuleta madhara makubwa na hata kufanya matukio mengine kutokea.



Jumbe za vyombo vya habari ambazo zinakemea vitendo vya ukatili na kukemea imani potofu za kishirikina, nina manufaa sana. Kwa kadiri ujumbe unavyosambaa, tunaona jamii ikikuza uelewa juu ya ualbino. Katika matukio ya hivi karibuni, taarifa hisi zinaibua shauku ya jamii kusaidia kuondoa uovu huu duniani. Tunapaswa kufanya kazi na vyombo husika kuzuia uvumi na kurekebisha makossa. Vyombo vya habari (kama vil redio) inaweza kuunganisha vikundi kusaidia kutafuta wahanga huku wakiwa hai katika eneo husika. Zingatia kuwaasa wanahabari **kutotaja thamani ya viungo vya watu wenye ualbino**, kwa kuwa kwa kufanya hivyo kunaongeza mauaji.

### Utafiti juu ya ualbino

Wakati wa kufanya utafiti au mahojiano juu ya ualbino, hakikisha ulinzi kamili wa data ya mahojiano ili wahojiwa wenye ualbino wasiweze kufuatwa.

Inawezekana kabisa katika kazi yako kama mtu unayehusika na Ulinzi au Meneja wa mradi vyombo vya habari vikawasiliana na wewe ili kupata maelezo ya ziada. **Tunashauri uwe makini kutambua ni nini unatoa kwa wanahabari. Ni vizuri ukatoa taarifa zinazoendana na taarifa rasmi iliyopo pale inapobidi.** Fanya kazi kwa makini na timu inayofuatilia tukio hilo.

**Epuka kutoa taarifa binafsi za mhanga au familia yake katika vyombo vya habari.** Unaweza ukafuatilia uhakika wa taarifa za ukatili na kuthibitisha mahali zilipotokea na **kuasa jamii kufuatilia na kumtafuta mhanga kwa kutoa maelezo ya jumla jumla** pekee. Tumia fursa vizuri unapokutana na vyombo vya habari kukemea Imani potofudhidi ya watu wenye ualbino

### Kutumia mitandao ya jamii pamoja na teknolojia

Katika ulimwengu wa sasa mitandao ya kijamii ndio mahali pa kwanza kupata taarifa endapo tukio la ukatili limetokea. Vyombo vya habari vya kawaida hupokea taarifa kutoka katika mitandao ya kijamii na kuanza uchunguzi wa kiina.

Iwapo taasisi yako ina mwitikio mkubwa katika mitandao ya kijamii, unaweza kutumia uwanda huu haraka kuripoti taarifa na upotevu wa mtu mwenye ualbino kwa watu wanaofuatilia mtandao wako. Omba msaada wa kumtafuta na toa taarifa kamili za mawasiliano na taarifa zote muhimu kuhusu upotevu. Teknolojia ya kisasa kama vile makundi ya whatsapp ni murua katika kusambaza taarifa. Nchini Malawi watu wenye ualbino wameunda makundi mahsusi ambapo wanashirikiana kwa taarifa muhimu.

### Kujifunza kutoka katika janga.

Bila kujali matokeao ya janga linapotokea, inashauriwa kufanya **tathmini ya jinsi janga lilivyo fanyiwa kazi baada ya tukio.** Hii itaongeza ufanisi wa taasisi yako katika kupanga na kuwa na weledi wa namna matukio yajayo

Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kwa watu wenye ualbino

yanaweza kusimamiwa. Pia iinaweza kusaidia kuzuia matukio mengine na kubadilishana uzoefu na taasisi zingine.

**Tenga muda kwa uaminifu na kufanya tathmini** ya mambo gani yalifanikiwa na yale ambayo hayakufanikiwa.

- Je taratibu zilizowekwa kulinda watu wenye ualbino zilifuatwa?
- Je mfumo wa mawasiliano ulikuwaje?
- Mambo yapi yalifanikiwa?
- Je uratibu wa rasilimali ulikuwa wa haraka?

Kutokea hapo, andaa mapendekezo madhubuti na usipotezee muda. Anza mara moja kutekeleza. Pia hakikisha kwamba unatoa mafunzo kwa watendakazi pale ambapo taratibu hazifuatwi vya kutosha.

-----  
Tunafuatilia kwa undani sana haki za watu wenye ualbino na hali ya ukatili wanayokabiliana nayo. Tunaamini kuwa chapisho hili litasaidia kukomesha uvamizi na kusaidia kulinda watu wenye ualbino.

Ulinzi na usalama kwa watu wenye ualbino una misingi ya kitamaduni. **Ni nafuu sana kutofautisha tamaduni** ambazo watu wenye ualbino wanatokea na kubaguliwa, pamoja na zile ambazo kipekee wanawindwa. Hii haimaanishi kuwa hatari hizi zinatokea sehemu zote.

Hasa hasa katika maeneo yengye migogoro na majanga, ambapo watu ambapo watu hikimbia kuokoa maisha yao na kile kidogo walichonacho wanachoweza kubeba. Watu wenye ualbino wapo katika hatari zaidi katika maeneo haya. Uwepo wa watu wenye ualbino unatakiwa kuingwa kwa uangalifu mkubwa kwa kupangilia **mfumo wa kukabiliana na majanga** na mfumo wa kutatua migogoro.



*Angalizo: "CBM, Christoffel-Blindenmission na Christian Blind Mission e.V. haitawajibika kutokana na matumizi yasiyo sahihi ya muongozo huu na haitahusika na namna muongozo huu utatumiwa.*



---

## **kwa maelezo Zaidi**

### **CBM**

Stubenwald-Allee 5  
64625 Bensheim  
Germany  
[www.cbm.org](http://www.cbm.org)

**CBM ni taasisi ya maendeleo ya kimataifa ya kikristo. CBM imejikita kuboresha ubora wa maisha kwa watu wenye ulemavu katika jamii maskini Zaidi unimwenguni.**